

FEEDING TAMPA BAY

**MPANGO WA MSAADA WA CHAKULA CHA DHARURA (TEFAP)
UTHIBITISHO WA KUSTAHIKI KUCHUKUA CHAKULA NYUMBANI
7 CFR 251**

Jina: _____

Idadi ya Watu Katika Kaya: _____

Anwani: _____

Jimbo: _____

Ifuatayo inaonyesha mapato ya kila mwaka kwa kila ukubwa wa familia. Ikiwa mapato yako ya kaya yako sawa au chini ya mapato yaliyoorodheshwa kwa idadi ya watu katika kaya yako, unastahiki kupokea chakula. **Chati iliyo hapa chini itaanza kutumika Julai 1, 2020 - Juni 30, 2021.**

Ukubwa wa Kaya	Mapato ya Mwaka	Mapato ya Mwezi	Mara mbili kwa Mwezi	Kila Wiki mbili	Mapato ya kila Wiki
1	\$16,588	\$1,383	\$692	\$638	\$319
2	\$22,412	\$1,868	\$934	\$862	\$431
3	\$28,236	\$2,353	\$1,177	\$1,086	\$543
4	\$34,060	\$2,839	\$1,420	\$1,310	\$655
5	\$39,884	\$3,324	\$1,662	\$1,534	\$767
6	\$45,708	\$3,809	\$1,905	\$1,758	\$879
7	\$51,532	\$4,295	\$2,148	\$1,982	\$991
8	\$57,356	\$4,780	\$2,390	\$2,206	\$1,103
Kwa kila mwanafamilia wa ziada ongeza:	\$5,824	\$486	\$243	\$224	\$112

Chati hii inaelezea viwango vya kustahiki mapato ya kila mwezi, mapato yanayopokelewa mara mbili kwa mwezi (malipo 24 kwa mwaka), mapato yanayopokelewa kila wiki mbili (malipo 26 kwa mwaka) na mapato ya kila wiki.

Unastahiki kupokea chakula kutoka kwa TEFAP ikiwa kaya yako inakidhi miongozo ya mapato iliyopo hapo juu au inashiriki katika programu zozote zifuatazo. Tafadhali weka alama kwenye nafasi karibu na kitengo kinachostahili.

_____ Ustahiki wa mapato

_____ Programu ya Msaada wa Lishe Bora (SNAP) (fka Vocha ya Chakula)

_____ Usaidizi wa Muda Mfupi kwa Familia Zinazohitaji Kusaidiwa (TANF)

_____ Mapato ya Ziada ya Usalama (SSI)

_____ Usaidizi wa Matibabu (Medicaid)

Tafadhali soma taarifa ifuatayo kwa uangalifu kisha utie sahihi kwenye fomu na uandike tarehe ya leo. Unahitaji tu kutimiza moja ya mahitaji haya ili ustahiki kupokea vyakula vya USDA.

Ninathibitisha kwamba mapato yangu ya mwaka ya jumla ya kaya yako sawa au chini ya mapato yaliyoorodheshwa kwenye fomu hii kwa kaya zilizo na idadi sawa ya watu AU kwamba ninashiriki katika programu ambazo nimetia alama kwenye fomu hii. Ninathibitisha pia kwamba hadi leo, ninaishi katika Jimbo la Florida. Uthibitisho huu unawasilishwa kwa uhusiano na upokeaji wa msaada wa Shirikisho. Maafisa wa programu wanaweza kuthibitisha kile nilichokithibitisha kuwa kweli. Ninaelewa kuwa kufanya uthibitisho wa uwongo kunaweza kusababisha kulazimika kulipa shirika la Serikali kwa thamani ya chakula kilichotolewa vibaya kwangu na kunitia mashtaka ya raia au ya jinai chini ya sheria za Serikali na Shirikisho.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

UTHIBITISHO HUU NI HALALI KWA MUDA WA MWAKA MMOJA na unaweza kufanywa upya kama inavyohitajika. Mabadiliko yoyote ya hali katika kaya ni lazima yaripotiwe kwa wakala wa usambazaji mara moja.

KWA HIARI: Ninamuidhinisha _____ kuchukua vyakula vya USDA kwa niaba yangu.

Kwa mujibu wa Sheria ya Haki za Raia na Shirikisho la Marekani. Sheria na sera za haki za raia za Idara ya Kilimo (USDA), USDA, Mashirika yake, ofisi, na wafanyikazi, na taasisi zinazoshiriki au kusimamia programu za USDA zimepigwa marufuku kubagua kwa msingi wa kijamii, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, ulemavu, umri au kulipiza kisasi kwa shughuli za awali za haki za raia katika mpango wowote au shughuli zilizofanywa au kufadhiliwa na USDA.

Watu wenye ulemavu ambao wanahitaji njia mbadala za mawasiliano kwa habari kuhusu mpango (k.v. Breli (maandishi ya vipofu), chapisho kubwa, kaseti, Lugha ya Ishara ya Marekani, n.k), wanapaswa kuwasiliana na Shirika (la Jimbo au mtaa) ambapo waliomba ruzuku. Watu ambao ni viziwi, walio na ugumu wa kusikia au wana shida ya kuzungumza wanaweza kuwasiliana na USDA kupitia Huduma ya Ruzuku ya Shirikisho kwa (800) 877-8339. Kwa kuongeza, maelezo ya programu yanaweza kupatikana katika lugha zingine isipokuwa Kiingereza.

Ili kuwasilisha malalamishi ya ubaguzi katika mpango, jaza [fomu ya Malalamishi ya Ubaguzi wa Programu ya USDA](#), (AD-3027) inayopatikana mtandaoni kwa: http://www.ascr.usda.gov/complaint_filing_cust.html, na katika ofisi yoyote ya USDA, au andika barua uielekeze kwa USDA na ueleeze kwenye barua habari zote zinazohitajika katika fomu hiyo. Ili kuomba nakala ya fomu ya malalamiko, piga simu (866) 632-9992. Wasilisha fomu yako iliyokamilika au barua kwa USDA kwa:

- (1) tuma barua kwa: Idara ya Kilimo ya Marekani
Ofisi ya Katibu Msaidizi wa Haki za Raia
1400 Independence Avenue, SW
Washington, D.C. 20250-9410;
- (2) faksi: (202) 690-7442; au
- (3) barua pepe: program.intake@usda.gov.

Taasisi hii inapeana fursa sawa.